

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
WIZARA YA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI

Anuani ya Simu: Elimu DAR ES
SALAAM


Simu: 110146-52

Telex: 41742 Elimu Tz.

Fax: 255-51-113271 Elimu Tz

Unapojibu tafadhali taja:

Kumb. Na. ED/OKE/NYE/VOL.1/06



S. L. P. 9121,

DAR ES SALAAM.

Tarehe: 27/04/2011

Makatibu Tawala wa Mikoa
Makatibu Tawala wa Wilaya
Wakaguzi Wakuu wa Shule wa Kanda
Wakaguzi wa Shule wa Wilaya
Wakuu wa Shule za Sekondari/Vyuo
Walimu Wakuu wa Shule za Msingi
TANZANIA BARA.

WARAKA WA ELIMU NA. 6 WA MWAKA 2011

KUPIGA MARUFUKU UTITIRI WA MITIHANI

Mtihani ni njia inayotumiwa kumwezesha mwalimu kujua kiwango cha uelewa wa wanafunzi kuhusu mada zilizofundishwa kwa kipindi fulani.

Kumezuka mtindo wa baadhi ya walimu kutunga mitihani mbalimbali na kuwapatia wanafunzi bila kuzingatia madhumuni ya mitihani katika mchakato mzima wa kujifunza. Walimu hao wanatunga mitihani na kuwapa wanafunzi wafanye kwa kulipia fedha kitendo hicho ni kinyume na taratibu na maadili ya ufundishaji.

Aidha, mitihani hii hufanyika kila mara kitendo kinachopunguza muda mwingi wa ufundishaji, mitihani hiyo ni kama: `speed test`, Mitihani ya Wiki, Mitihani ya Ujirani Mwema na Mitihani ya Mwezi. Mitihani yote hii wanafunzi huchanga fedha.

Ili kupunguza utitiri wa mitihani, Wizara inashauri mitihani ifuatayo ndio itiliwe mkazo.

- Mitihani ya Nusu Muhula
- Mitihani ya Muhula
- Mitihani ya Mwezi

Aidha, mitihani hii ifanyike bila kuchangisha fedha wanafunzi.

Kwa Waraka huu ninaagiza kuacha mara moja kuwapa wanafunzi mitihani inayotolewa bila lengo maalumu. Mazoezi ya darasani yatumike kupima uelewa wa mada zilizofundishwa.

Mwalimu yeyote atakayebainika akichangisha fedha kwa kisingizio cha kugharimia mitihani atachukuliwa hatua kali za kinidhamu.

Waraka huu unaanza kutumika mara moja.

Umesainiwa na:

M. M. Wassena

KAIMU KAMISHNA WA ELIMU

Nakala:

1. Katibu Mkuu, Ofisi ya Waziri Mkuu TAMISEMI
2. Wakurugenzi wote, Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi.